*Kioo cha Lugha, Juz. 20 (2), 239-256*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v20i2.6

# Dosari za Kisarufi za Wanafunzi Wanaojifunza Kiswahili Sanifu katika Vyuo Vikuu nchini Burundi

*Dieudonné Butoyi*[1] na *Zelda Elisifa*[2]

**Ikisiri**

Utafiti huu ulichunguza aina za dosari za kisarufi zinazofanywa na wanafunzi wanaojifunza Kiswahili sanifu kama lugha ya pili katika baadhi ya vyuo vikuu nchini Burundi. Data zilikusanywa kutoka kwa wanafunzi wanaosoma mwaka wa pili na wa tatu katika vyuo vikuu husika. Usampulishaji nasibu ulitumika kupata sampuli ya washiriki 80. Data zilikusanywa kwa njia za hojaji na upitiaji nyaraka. Matokeo yalionesha kuwa wanafunzi hufanya dosari mbalimbali za kisarufi katika makundi makubwa manne ya kisarufi ambayo ni: ya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Dosari hizi zinazotokana na athari za lugha za awali katika Kiswahili sanifu zilidhihirisha hali ya wanafunzi kutoweza kubainisha tofauti kati ya mifumo ya kisarufi ya lugha hizo za awali na ule wa Kiswahili sanifu.

## 1.0 Utangulizi

Kiswahili ni lugha ya Kibantu inayotumika Afrika Mashariki na ya Kati. Kwa mujibu wa KAKAMA (2019), Kiswahili hutumika katika jumuiya mbalimbali za Afrika. Lugha hii muhimu haikupewa kipaumbele katika nchi za Afrika ya Kati kama vile Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda na Burundi. Hivyo, baadhi ya vyuo vikuu vya Burundi vilipoanzisha programu za Kiswahili sanifu mwaka 2011, kazi za wanafunzi wanaojifunza Kiswahili sanifu kama lugha ya pili zilidhihirisha kutokea kwa mwingiliano wa lugha za awali na Kiswahili sanifu. Hali hii ilisababisha utokeaji wa dosari kwa wanafunzi wanapojifunza Kiswahili sanifu kama lugha ya pili.

Dosari zinazojitokeza, aghalabu katika lugha ya pili, zimefasiliwa na kujadiliwa na wataalamu mbalimbali wakiwamo Corder (1973); Selinker (1972); Richards (1974) na Ferris (2011). Kwa mujibu wa Ferris (2011:3), "Dosari katika lugha ni mifumo ya kimofolojia, kisintaksia na kileksikolojia inayotofautiana kabisa na kanuni za lugha ya pili ambayo inakiuka matarajio ya wazungumzaji wazawa." Naye Corder (1981) anaeleza dosari kama upungufu wa kimfumo uliosababishwa na ukosefu wa umilisi wa lugha kwa wanaojifunza. Aidha, katika

[1] Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu cha Burundi, Burundi. Baruapepe: Baruapepe: dbutoyi17@gmail.com
[2] Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Baruapepe: zemmangare@gmail.com

mazingira ya ujifunzaji wa lugha ya pili, wataalamu mbalimbali, wakiwamo Lee (2001) na Zhang (2007), huona kuwa lugha ya pili huathiriwa na lugha ya kwanza ambayo mwanafunzi au mjifunzaji alilelewa nayo. Hivyo, kutokea kwa dosari kwa mwanafunzi au mjifunzaji wa lugha ya pili hutokana na lugha ya kwanza.

Kama ilivyo kawaida ya lugha, kutokana na kukua na kupanuka kwa matumizi ya Kiswahili sanifu katika mazingira rasmi na yasiyo rasmi, Kiswahili kimeendelea kuathiriwa na lugha za kijamii au lahaja za Kiswahili zinazozungumzwa na jamii mbalimbali kinamotumika. Hivyo, lengo la makala hii ni kubaini aina za dosari za kisarufi zinazofanywa na wanafunzi wanapojifunza Kiswahili sanifu katika vyuo vikuu vya Burundi.

## 2.0 Maandishi Tangulizi kuhusu Dosari za Kisarufi katika Ujifunzaji wa Lugha ya Pili

Tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusiana na dosari zinazojitokeza katika ujifunzaji wa lugha ya pili ambazo zilishughulikia maandishi ama mazungumzo. Aidha, tafiti hizo zinahusu nyanja tofauti za lugha, mathalani, fonolojia, mofolojia, sintaksia, leksikolojia na sematiki. Katika muktadha wa ujifunzaji lugha ya pili, baadhi ya tafiti zinadhihirisha kuwa dosari hutokana na sababu mbalimbali, hasa athari za lugha ya kwanza. Kwa mfano, Jabeen na wenzake (2015) walipotafiti dosari za wanafunzi wa vyuo vikuu vya Pakistani na Irani wanaojifunza Kiingereza kama lugha ya pili waligundua kuwa dosari nyingi za kisarufi huhusu matumizi mabaya ya nyakati za vitenzi. Naye Cioroianu (2015) alitafiti dosari za wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiromania na kuonesha kuwa dosari za wanafunzi hupatikana katika viwango vya fonetiki, msamiati, mofolojia na sintaksia.

Katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili, baadhi ya tafiti zilishughulikia dosari za kisarufi zinazotokana na athari za lugha za kijamii au lahaja nyingine za Kiswahili katika Kiswahili sanifu. Oduor na wenzake (2017) walishughulikia dosari zinazotokana na athari za uhamishaji wa sintaksia ya Kiluo katika upatanishi wa kisarufi wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa Kenya ambao lugha yao ya kwanza ni Kiluo. Katika utafiti huo, waling'amua kuwa kuna viwango vitatu vya kisarufi vilivyoathiriwa kutokana na uhamishaji wa sarufi ya Kiluo kwenda sarufi ya Kiswahili sanifu. Viwango hivyo ni vya ngeli, nafsi na idadi. Mpangala (2018) aliposhughulikia athari ya lugha ya Kimakonde katika kujifunza lugha ya Kiswahili aligundua matatizo ya kimatamshi, kimsamiati na kimaana. Naye Nyanda (2015) alitafiti athari za lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili na alibainisha dosari za kimsamiati, kimatamshi na kimaana. Aruba na wenzake (2017) walichanganua dosari za kisemantiki zinazojitokeza katika mawasiliano andishi ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za upili nchini Kenya. Matokeo ya kazi yao yanaonesha kuwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili wanatumia msamiati usiofaa, wanaunganisha maneno visivyo na kurundika maneno katika sentensi. Chepkwony (2011) aliyetafiti matatizo ya kisarufi ya wanafunzi wa Kikipsigis wanaojifunza Kiswahili sanifu

alijikita tu katika matatizo ya kimofolojia na kisintaksia. Matokeo ya utafiti huo yalidhihirisha kuwa dosari nyingi za kisarufi hutokana na athari za lugha ya Kikipsigis. Mtafiti aliona pia kuwa dosari hizi huhusu ujumlishaji mno wa baadhi ya maumbo ya sarufi ya Kiswahili sanifu.

Pia, Bundalla (2017) alitafiti athari ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu na matokeo ya utafiti wake yalidhihirisha kuwa Kiswahili sanifu huathiriwa na matumizi ya matamshi, maumbo ya msamiati na msamiati wenyewe wa Kimakunduchi. Kwa mfano, Kimakunduchi hudondosha nazali katika msamiati wake inapokutana na sauti [pj] na kikwamiza [ʧ]. Pia, utafiti ulionesha kuwa nazali hudondoshwa zinapofuatana na vikwamiza ghuna kama vile [z], na [v] katika baadhi ya msamiati. Hivyo, maneno ya Kiswahili kama vile *mnyama, mpya, mvua, nchi* na *nzi* hutamkwa *nyama*, *pya*, *vua*, *chi* na *zi*, mtawalia. Aidha, ilidhihirika kuwa baadhi ya msamiati wa Kimakunduchi unafanana na wa Kiswahili sanifu. Hii pia ni sababu ya kukwamisha mawasiliano kwa wazungumzaji wa Kimakunduchi wanapoongea Kiswahili sanifu. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa msamiati huo ni pamoja na majina ya walemavu, koo, siku, nyakati na msamiati wa kazi ambazo hufanywa na jamii husika.

Naye Ame (2017) alitafiti athari za kiisimu za lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili sanifu. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa wazawa wa Kitumbatu wanapotumia Kiswahili sanifu huathiriwa na lahaja ya Kitumbatu katika nyanja za msamiati, mazungumzo, maandishi na maumbo ya maneno. Pia, ukosefu wa vitabu vya kufundishia, wanafunzi kutumia Kitumbatu madarasani kuliko Kiswahili sanifu, kutokuwa na ujuzi wa kutosha wa sarufi ya Kiswahili sanifu na umbali wa kijiografia kati ya Tumbatu na Unguja zilibainika kuwa sababu za athari hizo katika Kiswahili sanifu.

Maandiko yaliyojadiliwa hapo juu yamedhihirisha kufanyika kwa tafiti mbalimbali kuhusu dosari zinazojitokeza kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili baada ya kuiamili lugha mama. Pia, maandiko hayo yamedhihirisha kuwa matumizi ya lugha ya pili kwa wanafunzi huathiriwa na lugha ya kwanza. Hivyo, wanafunzi wa lugha ya pili hufanya dosari katika mazungumzo au maandishi yao ambazo kwa kiasi kikubwa hutokana na athari za lugha ya kwanza. Dosari hizo zinajitokeza katika viwango vya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki.

Utafiti huu umejikita katika kutathmini aina za dosari za kisarufi za wanafunzi wa lahaja ya Kingwana wanaojifunza Kiswahili sanifu kama lugha ya pili katika vyuo vikuu vya Burundi. Tofauti na tafiti zilizoelezwa hapo juu, utafiti huu ulishughulikia dosari za kisarufi kwa ujumla zinazotokana na athari za lahaja ya Kingwana katika Kiswahili sanifu. Imebainika kuwa dosari za aina mbalimbali zinajitokeza katika viwango vya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki.

**3.0 Nadharia ya Utafiti**

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa iliyoasisiwa na Stephen Pit Corder (1967) ili kutambua na kuainisha makosa na kufafanua chanzo chake. Hii inadhihirisha kuwa nadharia hii inatumika kuchunguza jinsi gani makosa katika lugha yanaweza kushughulikiwa. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa, baadhi ya makosa yanayofanywa na wanafunzi wanapojifunza lugha ya pili hutokana na athari za lugha ya kwanza. Ijulikane kuwa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ilitokea kuwa kibadala cha Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi iliyoasisiwa na Fries (1945) na kuendelezwa na Robert Lado (1957). Kwa mujibu wa Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi, uchanganuzi wa makosa ulikuwa kazi ya ulingalishi wa mifumo sahihi ya lugha moja na nyingine, yaani lugha mama ya mwanafunzi na lugha ya pili anayojifunza (Ntawiyanga, 2018). Tofauti na Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi, Nadharia ya Uchanganuzi Makosa inazingatia kuwa makosa yanayofanywa na mwanafunzi katika kujifunza lugha ya pili ni ishara kwamba ametilia mkazo kujifunza na kuelewa kanuni za lugha hiyo. Isitoshe, Nadharia ya Uchanganuzi Makosa inaelekeza kuwa makosa katika lugha yanaweza kuchunguzwa na kuainishwa kulingana na kiwango cha lugha. Hivyo, yanapatikana makosa ya kifonolojia, kimofolojia, kimsamiati, kisintaksia na kisemantiki.

Kama inavyoelezwa na Corder (1974), Nadharia ya Uchanganuzi Makosa inaweza kutumiwa kwa kufuata hatua tano. Hatua hizo ni: (1) kukusanya data, (2) kutambua makosa, (3) kuainisha makosa, (4) kueleza makosa, na (5) kutathmini makosa. Kutokana na hatua hizi, ni dhahiri kuwa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa inaweza kutoa picha ya aina za makosa ya wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili. Kukusanya data, kutambua, kuainisha, kueleza na kutathmini makosa ni njia mwafaka zinazomwongoza mtafiti katika kuchakata makosa ya wanafunzi wa lugha ya pili. Isitoshe, Nadharia ya Uchanganuzi Makosa inaweza kusaidia walimu katika kushughulikia na kusahihisha makosa ya wanafunzi, pamoja na kuwaelekeza wanafunzi ili kuzuia utokeaji wa makosa wanapojifunza lugha ya pili. Kuelewa mifumo ya lugha ya kwanza na ya pili ni jambo muhimu katika kuchakata, kuchambua na kufafanua makosa kwa msingi wa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Hata hivyo, katika muktadha wa utafiti huu, dosari katika matumizi ya lugha zimechukuliwa sawa na makosa katika lugha hiyo kwa kigezo cha wingi wa utokeaji wa aina ya dosari hiyo, kama ilivyo kwa Nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa.

## 4.0 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika vyuo vikuu vitano nchini Burundi. Vyuo hivyo ni Chuo Kikuu cha Burundi (Université du Burundi, U.B), Chuo Kikuu cha Busara ya Afrika (Université Sagesse d'Afrique, USA), Chuo Kikuu cha Mwanga cha Bujumbura (Université Lumière de Bujumbura, ULBu), Chuo Kikuu cha Maziwa Makuu (Université des Grands Lacs, UGL) na Chuo Kikuu cha Mwaro (Université de Mwaro, UM). Uteuzi wa vyuo hivi ulizingatia kigezo kwamba ni vyuo vinavyofundisha Kiswahili kama kozi ya lazima katika miaka miwili au mitatu ya shahada ya kwanza.

Katika utafiti huu, wanafunzi 80 wanaosoma Kiswahili mwaka wa pili na wa tatu katika vyuo tajwa walishirikishwa. Wanafunzi 16 kutoka katika kila chuo walipatikana kwa njia ya usampulishaji nasibu ambapo wanafunzi wote wanaosoma Kiswahili sanifu katika kila chuo walikuwa na nafasi sawa ya kushiriki. Wote walipewa karatasi 16 zilizoandikwa namba 1 hadi 16. Karatasi hizo zilichanganywa na nyingine zisizo na namba 19 ambazo zilifikia jumla ya karatasi 35. Kila mmoja aliokota karatasi moja na wale waliookota karatasi zenye namba tu, ndio walioshiriki katika utafiti huu. Data zilipatikana kwa kutumia mbinu mbili tofauti. Kwanza, ni mapitio ya nyaraka ambazo kwa muktadha huu ni insha zilizoandikwa na watoataarifa. Watafiti walipitia kazi mbalimbali za maandishi zilizofanywa na wanafunzi, hasa wa mwaka wa pili na wa tatu. Pia, walitambua na kuhesabu dosari hizo ili kuzibainisha kiidadi kutokana na aina zake. Pili, watafiti walitumia hojaji yenye maswali-funge na wazi ili kupata taarifa iliyotarajiwa. Njia hii ilitumika ili kushadidia matokeo ya njia ya kwanza ya upitiaji wa nyaraka.

## 5.0 Matokeo ya Utafiti

Kama ilivyokwishaelezwa, utafiti huu umejikita katika ubainishaji wa aina za dosari zinazotokea katika Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wa vyuo vikuu vya Burundi. Pamoja na kulitekeleza jambo hilo, ilibainika pia namna ambavyo lugha ya awali huathiri Kiswahili sanifu. Data za watoataarifa 80 zilichambuliwa ili kudhihirisha aina za dosari zinazofanywa na wanafunzi ambao lugha mama kwao siyo Kiswahili. Jedwali Na. 1 linaonesha bayana matokeo ya utafiti huu kwa kubainisha aina za dosari zilizopatikana katika matumizi ya Kiswahili sanifu kutokana na athari za lugha ya awali:

**Jedwali Na. 1: Aina za Dosari katika Kiswahili Sanifu kutokana na Lugha ya Awali**

| Na. | Dosari | Idadi ya Utokeaji | Jumla | % |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Udondoshaji wa Fonimu | 99 | 691 | 14.32 |
| 2. | Ubadilishanaji wa Fonimu | 67 | “ | 9.69 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3. | Uzalishaji wa Fonimu | 69 | " | 9.98 |
| 4. | Upatanisho kati ya Nomino na Kitenzi | 24 | " | 3.47 |
| 5. | Upatanisho kati ya Nomino na Nomino | 52 | " | 7.52 |
| 6. | Udondoshaji wa Viambishi Vinavyofaa | 38 | " | 5.49 |
| 7. | Ongezeko la Viambishi Visivyofaa | 78 | " | 11.28 |
| 8. | Matumizi ya Viambishi Visivyofaa | 41 | " | 5.93 |
| 9. | Ugeukaji wa Viambishi Tegemezi kuwa Neno | 40 | " | 5.78 |
| 10. | Kuunganisha Maneno Visivyo | 21 | " | 3.03 |
| 11. | Kukata Maneno Visivyo | 68 | " | 9.84 |
| 12. | Matumizi ya Msamiati Usiosahihi | 94 | " | 13.60 |

**Chanzo:** Uwandani (2020-2021)

Jedwali Na. 1 linaonesha aina za dosari ambazo zimejadiliwa katika sehemu zinazofuata. Aidha, linaweka bayana kiasi cha dosari kutokana na kila aina ya dosari.

### 5.1 Udondoshaji wa Fonimu

Udondoshaji wa fonimu ni hali ya kuondoa kipashio fulani cha kiisimu katika silabi au neno (Matinde, 2012). Data zimedhihirisha kwamba wanafunzi wanaojifunza Kiswahili sanifu kama lugha ya pili hudondosha baadhi ya fonimu katika maneno ya Kiswahili sanifu yenye fonimu hizo wanapotakiwa kuyazungumza au kuyaandika katika kazi zao. Tungo zifuatazo kutoka katika matini za wanafunzi zinathibitisha hayo:

1. (a) *Nimekutana na magali mengi balabalani *ivo* nimefika *apa* chuoni.
   → Nimekutana na magari mengi barabarani, hata *h̲ivyo* nimefika *h̲apa* chuoni
   (b) *Nimeludiya *apa* darasani kusoma mpaka sasa *ivi*.
   → Nimerudi *h*apa darasani ili (niweze) kusoma hadi sasa *h̲ivi*.
   (c) *Mungu alitulinda, *atukufanya ata* ajali moja.
   → Mungu alitulinda, *h̲atukufanya h̲ata* ajali moja.
2. (a) *Safari yangu leo *imekua* nzuri sana.
   → Leo safari yangu *imekuw̲a* nzuri sana.
   (b) *Nimekutana na rafiki yangu *ambae* tunasoma *nae*.
   → Nimekutana na rafiki yangu *ambay̲e* tunasoma *nay̲e*.

Katika sentensi 1 (a), 1 (b) na 1 (c) ilidondoshwa fonimu /h/. Hali hii ni kutokana na kwamba katika mazungumzo ya kawaida, watoataarifa huiacha fonimu hiyo mara wanapotamka leksimu zinazohusisha fonimu hiyo. Hivyo, imedhihirika kuwa udondoshaji wa fonimu huathiri Kiswahili sanifu pale ambapo fonimu /h/ hulazimika kuwapo ama katika mazungumzo au maandishi. Katika sentensi 2(a)

na 2 (b), fonimu /j/ na /w/ zilidondoshwa kutoka katika maneno _ambaye_ na _kuwa_. Kwa kuwa lugha za awali za watoataarifa huzalisha fonimu nusu irabu /j/ na /w/ pale ambapo Kiswahili sanifu huhusisha mfuatano wa irabu mbili, wanafunzi wa lugha hizo hawakuweza kubainisha utokeaji wa fonimu /j/ na /w/ wala kutokuwapo kwake katika Kiswahili sanifu, kama vile katika maneno *_ambae><ambaye_ na _*kua><kuwa._

**5.2 Ubadilishaji wa Fonimu**

Fonimu za Kiswahili huwa ni zilezile zinazohusika katika lugha za Kibantu zilizoko katika maeneo wanakotoka watoataarifa. Ufanano huo unasababisha hali ya ubadilishaji wa fonimu. Baadhi ya sentensi zilizonukuliwa kutoka katika insha za wanafunzi zimedhihirisha ubadilishaji wa fonimu katika maneno ya Kiswahili sanifu kama yafuatayo:

3. (a) *Nimekutana na _magali_ mengi _balabalani_ ivo nimefika apa chuoni.
→ Nilipokuwa _barabarani_, nimekutana na _magari_ mengi; hivyo ndivyo nilivyofika hapa chuoni.
(b) *_Nilijitayalisha_ ili nikuje chuoni.
→ _Nilijitayarisha_ kwa ajili ya kuja/kufika chuoni.
4. (a) *Kufikisha muda huu nimevumiliya na kusikiliza _mwarimu_.
→ Hadi sasa, nimevumilia nikimsikiliza _mwalimu_.
(b) *Nimechukua vyombo vyangu _vya shure._
→ Nimechukua vifaa vyangu vya _shule_.
5. (a) *_Ni mepiga_ chayi.
→ _Nimepika_ chai.
(b) *Njiani nimeenda _gusoma_ nimepita chooni.
→ Njiani nikienda _kusoma_ nimepita chooni.
6. (a) *_Nimechika_ njia kwenda kanisani.
→ (_Nimeshika..._) Nimeelekea kanisani.
(b) *Padri akaingiya _kicha_ akaanza mafundisho.
→ Padri akaingia _kisha_ akaanza mahubiri.

Katika 3 (a) na (b), 4 (a) na (b) ulibainika ubadilishaji wa fonimu /l/ kuwa /r/. Hii ilitokana na kwamba katika baadhi ya maeneo, lugha ya Kiswahili iliathiriwa na lugha zinazopakana nayo zinazohusisha fonimu /r/, kama vile Kirundi na Kinyarwanda. Hivyo, watoataarifa hushindwa kutambua mazingira ambamo /r/ au /l/ zinatumiwa. Katika 5 (a) na 5 (b) kulitokea ubadilishaji wa fonimu /k/ kuwa /g/. Hii ilitokana na athari za lugha zinazopakana na Kiswahili, kama vile Kirundi na Kinyarwanda. Lugha hizo huhusisha kanuni ya kimofofonolojia ya usigano ambapo fonimu mbili ambazo si ghuna haziwezi kufuatana kwenye mipaka ya mofu. Kuhusu 6 (a) na 6 (b), wanafunzi walitumia /ʧ/ (ch) badala ya /ʃ/ (sh). Hii ni athari ya Kifaransa. Nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, lugha ya Kiswahili iliathiriwa sana na Kifaransa, hivyo, wanafunzi kutoka nchi hiyo

hushindwa kubainisha /ʃ/ ya Kifaransa (ch: kwa unukuzi wa kawaida) na /ʃ/ itumikayo katika Kiswahili sanifu (sh: kwa unukuzi wa kawaida).

**5.3 Uzalishaji wa Fonimu**

Uzalishaji wa fonimu ni mchakato ambao fonimu fulani inajitokeza mahali ambapo haikuwapo. Mfuatano wa fonimu usio sawa kati ya lugha mbalimbali zinazopakana na Kiswahili husababisha uzalishaji au uchopekaji wa fonimu ambazo zisingekuwapo katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu. Sentensi zifuatazo zilizonukuliwa kutoka katika insha za wanafunzi zinadhihirisha hali hiyo:

7. (a) **Akaniambiya* mwanangu usiache masomo.
→ *Akaniambia*: mwanangu usiache shule.
(b) **Tuliongeya* sana baada ya hapo nikaja shuleni.
→ *Tuliongea* sana baadaye nikaelekea shuleni.
(c) *Mwenyezi Mungu yeye *alionilamusha*.
→ Mwenyezi Mungu ndiye *aliyeniamsha*.
(d) **...kujuwa* namna *yakutatuwa* tatizo fulani fulani.
→ *...kujua* namna *yakutatua* tatizo fulani fulani.
8. (a) *Elimu inasaidia *mutu (...)*
→ Elimu inasaidia *mtu (...)*
(b) **Nimeamuka* asubuhi mapema sana nikajiandaa ili niende.
→ *Nimeamka* asubuhi mapema sana nikajiandaa kwenda/ kuondoka.
9. (a) *Nilikuta bado wanafunzi wapo *inje*.
→ Niliona bado wanafunzi wapo *nje*.
(b) *Jambo la *inne* na la mwisho (...).
→ Jambo la *nne* na la mwisho (...).
(c) *Elimu ni muhimu katika *inchi* juu inasababisha *inchi* isonge mbele.
→ Elimu ni muhimu *nchini* kwani huisababisha *nchi* kusonga mbele/kupata maendeleo.

Sentensi 7 (a), 7 (b), 7 (c) na 7 (d) kati ya irabu moja na nyingine kulizalishwa konsonanti. Kama ilivyokwishaelezwa, lugha ya Kiswahili iliathiriwa sana na lugha za awali za watoataarifa ambazo hazihusishi mfuatano wa irabu mbili katika neno moja. Hivyo, baina ya /i/ na /a/ au /e/ na /a/ kumeingizwa /j/ (*Akaniambia*><**Akaniambiya, Tuliongea* ><**Tuliongeya*). Kwa upande mwingine, baina ya /i/ na /a/ kuliwekwa /l/ (*aliyeniamsha*><**alionilamusha*). Katika 8 (a) na 8 (b) kulizalishwa fonimu irabu /u/ baina ya konsonanti halisi mbili /m/ na /t/ (*mtu*><**mutu*), au /m/ na /k/ (*Nimeamka*><**Nimeamuka*). Tatizo hili hutokana na kwamba lugha za awali zilizoathiri Kiswahili hazihusishi mfuatano wa konsonanti mbili zinazotamkika katika mafungu mawili tofauti. Hivyo, wanafunzi wanapotamka au kuandika maneno ya Kiswahili kama *mtu*, *kutamka*, *mkia*, *mti*, na *mpira*, huzalisha irabu kati ya konsonanti mbili zinazofuatana. Kwa

upande mwingine, ni dhahiri kuwa lugha zilizoathiri Kiswahili hudumisha mfumo wa silabi wa KI. Katika 9 (a), 9 (b) na 9 (c) kulijitokeza fonimu /i/ kwenye maneno *nje, nne* na *nchi*. Maneno yote haya huhusisha fonimu /n'/ inayojibainisha kimatamshi na *je, ne* na *chi*. Kutokuwapo kwa fonimu hiyo katika abjadi ya lugha mbalimbali za kijamii zilizoathiri Kiswahili (Kirundi, Lingala, Chiluba, Kishi, n.k.), kulisababisha utokeaji wa /i/ na hivyo kuidhoofisha fonimu /n'/ katika Kiswahili. Kwa hiyo, watoataarifa waongeapo Kiswahili sanifu huweka fonimu /i/ mwanzoni mwa maneno yanayohusisha fonimu /n'/.

## 5.4 Upatanisho wa Kisarufi

Upatanisho wa kisarufi ni mbinu ya kuoanisha maneno ili yawiane vizuri kisintaksia. Dosari za upatanisho wa kisarufi za aina tofautitofauti zilidhihirika katika insha zilizotungwa na wanafunzi. Dosari hizo zimebainishwa katika sehemu ndogondogo zifuatazo:

### 5.4.1 Upatanisho wa Nomino na Kitenzi

Katika upatanisho wa kisarufi kati ya nomino na kitenzi, vipo viambishi ngeli ambavyo hudhihirisha upatanisho wa kisarufi, yaani maneno hayo huwiana na kutoa ujumbe kamili. Sentensi zifuatazo ambazo zilinukuliwa kutoka katika insha za wanafunzi zinadhihirisha ukiukaji wa kanuni za upatanisho wa kisarufi baina ya nomino na kitenzi kwa kuhusisha kiambishi ngeli kisichoendana na nomino husika.

10. (a) *Gali *ikanifikisha* mjini.
    → Gari *likanifikisha* mjini.
    (b) *Mahubiri *ilipofika* mwisho, tulimuabudu tena Mungu kwa nyimbo.
    → Mahubiri *yalipofika* mwisho (...)→ Mahubiri *yalipoisha*, (sahihi)
    (c) *Kila kabila *ina* utamaduni yao.
    → Kila kabila *lina* utamaduni wake.
11. (a) *Simba *iliuliwa* na askari polisi.
    → Simba *aliuawa* na askari polisi.
    (b) *Nguruwe zetu *zinaishi* kibandani.
    → Nguruwe wetu *wanaishi* kibandani.
12. (a) *Elimu *unasadia* katika maisha.
    → Elimu *inasadia* katika maisha.
    (b) *Elimu mzuri *atufungulia* mlango wa kazi.
    → *Elimu* nzuri *inatufungulia* mlango wa kazi.
    (c) *Kazi yake tangu *aliezaliwa* ni kufuga.
    → Kazi yake tangu *alipozaliwa* ni kufuga.

Katika 10 (a), 10 (b) na 10 (c) kiambishi kipatanishi cha ngeli kilichotokea kwenye vitenzi vyote huwa ni {i-} badala ya {li-}, {ya-} na{li-}. Dosari hii hujitokeza sana kwa wanafunzi wasomapo Kiswahili sanifu kwa sababu katika lugha zao za awali

upo uwezekano wa wazungumzaji kuhusisha ngeli ya I-ZI badala ya ngeli nyingine yoyote. Suala hili hujitokeza hasa kwa wazungumzaji wa Kiswahili cha Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Kuhusu 11 (a) na 11 (b), wanafunzi walikosea kwa sababu lugha zao za awali hutofautisha nomino za wanyama na za watu. Nomino za wanyama huwekwa katika ngeli ya I-ZI na za watu katika ngeli ya A-BA. Ikumbukwe kuwa Kiswahili sanifu hujumuisha nomino za watu na za wanyama katika ngeli moja ya A-WA. Katika 12(a), 12(b) na 12 (c), jinsi vipatanishi vilivyotumiwa kuhusiana na nomino moja inadhihirisha kuwapo kwa wanafunzi ambao ngeli za lugha zao za awali zilichukua nafasi kubwa kuliko zile za Kiswahili sanifu.

### 5.4.2 Upatanisho kati ya Nomino/Kiwakilishi na Kivumishi

Kivumishi cha Kiswahili, kama ilivyo katika lugha za Kibantu, huambikwa viambishi ngeli kutokana na nomino husika. Ina maana kuwa, kiambishi ngeli cha nomino hupatikana tena kwenye kivumishi cha nomino hiyo. Katika mchakato wa uwiano wa nomino na kivumishi, dosari zinazohusiana na uambatanishaji wa nomino na kivumishi zilitokea katika baadhi ya insha za wanafunzi. Hebu tutazame sentensi zifuatazo zilizotungwa na wanafunzi:

13. (a) *Kwa namna *ingine*, ninaweza kusema kuwa elimu inasaidia(...).
→ Kwa namna *nyingine*, ninaweza kusema kuwa elimu husaidia (...).
(b) *Nikaosha kinywa na *mwili zima*.
→ Nikapiga mswaki na kuoga mwili *mzima*.
14. (a) *Polisi njiani walisimamisha *basi yetu*.
→ Njiani, polisi walisimamisha basi *letu*.
(b) *Kila kabila ina utamaduni *yao*.
→ Kabila lolote lina utamaduni *wake*.
15. (a) *Mtu alie kuwa na *elimu mzuri*.
→ Mtu aliyekuwa na elimu *nzuri*.
(b) *Baba mzazi akanituma kumuletea *beskeli lake*.
→ Baba mzazi akanituma kumletea *baiskeli yake*.

Katika 13 (a) na 13 (b), vivumishi *ingine* na *zima* havikuambikwa viambishi vinavyodhihirisha upatanisho wa kisarufi baina yake na nomino husika. Kuhusu kivumishi *ingine*, watoataarifa walitumia {(y)i-} pale ambapo kiambishi kipatanishi kingekuwa {*ny*-}. Kuhusu 13 (b), kutokea kwa *zima* bila kipatanishi kulisababishwa na mwanafunzi kutotambua kanuni za upatanisho wa kisarufi baina ya nomino na kivumishi. Katika tungo 14 (a) na 14 (b), vivumishi *-etu* na *-ao* vimeambikwa kipatanishi {i-}. Katika baadhi ya lugha za awali za watoataarifa, ngeli ya I-ZI hutumika mara kwa mara badala ya ngeli nyingine. Hivyo, katika matumizi ya Kiswahili sanifu wanafunzi waliathiriwa na mifumo ya upatanisho ipatikanayo katika lugha za awali za wanafunzi. Katika 15 (a) na 15 (b), vivumishi *-zuri (mzuri)* na *-ake (lake)* viliambikwa viambishi visivyohusiana na nomino

husika (elimu, *beskeli><baiskeli). Kutokana na maelezo yaliyotolewa hapo juu, upatanisho wa kisarufi baina ya nomino na kivumishi haukuzingatiwa.

### 5.5 Udondoshaji wa Viambishi

Katika sentensi mbalimbali zilizotungwa na wanafunzi, dosari zinazohusiana na udondoshaji wa viambishi ambavyo vingekuwapo zilitokea. Sentensi zifuatazo ni mifano inayodhihirisha dosari za aina hiyo:

16. (a) *Wakati *tulifika* pande la soko ya COTEBU... (tulipofika)
→ Wakati *tulipofika* karibu na soko la COTEBU...
(b) *Kwa bahati nzuri hakuna mtu *aliumia*. (aliyeumia)
→ Kwa bahati nzuri hakuna mtu *aliyeumia*.
17. (a) *Niliwasalimia *rafiki* zangu. (marafiki)
→ Niliwasalimia *marafiki* zangu.
(b) *Inatubidi kuelimishwa ili tupate kufanyikisha *lengo zetu*.
→ Inatubidi kuelimishwa ili tupate kufanikisha *malengo yetu*.
18. (a) *Elimu inatusaidia *kuweza ichi* na watu (Kuweza kuishi)
→ Elimu inatuwezesha *kuishi* na watu wengine.
(b) *Aliepata elimu anafaidika kuliko yule *hajawahi elimika*.
→ Aliyepata elimu anafaidika kuliko yule ambaye *hajawahi kuelimika (hajaelimika)*.

Katika sentensi 16 (a) na 16 (b) viambishi rejeshi {-*po*-} na {-*ye*-} vilidondoshwa kutoka katika vitenzi (**tulifika*>< *tulipofika, *aliumia*>< *aliyeumia*). Watafiti walitambua kuwa watoataarifa ambao baadhi yao walikuwa ni Waswahili wa Burundi au wa nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo hudondosha viambishi rejeshi wanapozungumza Kiswahili. Hivyo, imedhihirika kuwa viambishi rejeshi havihusishwi katika lugha ya awali wala Kiswahili kitumikacho katika nchi hizo. Katika 17 (a) na 17 (b) vilidondoshwa viambishi vya wingi kutoka katika nomino husika (**rafiki*><*marafiki, *lengo*><*malengo*). Hivyo, nomino *marafiki* ya A-WA na nomino *malengo* ya LI-YA ziliondolewa kiambishi cha wingi *ma*- na kuingizwa katika ngeli ya I-ZI. Kwa sababu hiyo, vivumishi vilivyoshirikiana na nomino hizi viliambikwa viambishi ngeli kutokana na ngeli ya I-ZI. Kuhusu 18 (a) na 18 (b) kiambishi {*ku*-} kilidondoshwa kutoka katika vitenzi *kuishi* na *kuelimika* (*kuweza *ichi*><kuweza *kuishi, hajawahi *elimika*><*hajawahi kuelimika*). Katika baadhi ya lugha za awali, kikiwamo Kiswahili cha Burundi na cha Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, kitenzi kikuu kinapotumika pamoja na kitenzi kisaidizi, kitenzi kikuu hupoteza kiambishi *ku*-. Hii imekuwa sababu ya watoataarifa kukiondoa kutoka katika vitenzi kinakohitajika pale wanapozungumza Kiswahili sanifu.

## 5.6 Uongezaji wa Viambishi

Dosari za uongezaji wa viambishi zilitokea pale ambapo wanafunzi walipachika viambishi au mofu ambazo kwa kawaida zisingekuwapo katika muktadha husika. Sentensi zifuatazo zinadhihirisha dosari za aina hii:

19. (a) *Niliamka *nikakula*.
→ Niliamka, *nikala*.
(b) *Usiache masomo ili *usikuwe* kama mimi.
→ Usiachane masomo ili *usiwe* kama mimi.
(c) *Basi ilikuya nikapanda *tukakuya*.
→ Basi lilikuja nikapanda *tukaja*.
20. (a) *Hio siku *ilikuwaga* siku ya shangwe kweli.
→Hiyo siku *ilikuwa* siku ya shangwe kweli.
(b) *Watoto bengi *balichezaga* mupira.
→ Watoto wengi *walicheza* mpira.
21. (a) *Ata *wa mama*, *wa baba, wa kaka, wa dada* wanaitaji kuwa na elimu.
→ Hata *mama, baba, kaka* na *dada* wanahitaji kuwa na elimu.
(b) *Nimesalimiya *wajamani bangu*.
→ Nimewasalimia *Øjamaa zangu*.
(c) *Wazazi wengi upeleka watoto wao mu *mashule.*
→ Wazazi wengi hupeleka watoto wao *shuleni*.

Katika sentensi 19 (a), 19 (b) na 19 (c) kiambishi {-*ku*-} kilipachikwa katika vitenzi *kula* (**nikakula*><*nikala*), *kuwa* (**usikuwe*><*usiwe*) *na kuya (kuja)* (**tukakuya*><*tukaja*), ambavyo ni vya silabi moja. Katika Kiswahili sanifu, vitenzi vya aina hii vinapotumika katika hali ya mfuatano wa matendo inayodhihirishwa na kiambishi {-*ka*-}, kiambishi {*ku*-} hudondoshwa. Hata hivyo, mfumo wa {*ka*-} kufuatana na {*ku*-} ni wa kawaida katika lugha ya awali hasa Kiswahili cha Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Burundi. Hivyo, wanafunzi walioathiriwa na mifumo ya kisarufi ya lugha za awali hudhihirisha matumizi ya kiambishi {*ku*-} pale ambapo kingeondolewa katika vitenzi vyenye silabi moja. Kuhusu 20 (a) na 20 (b) wanafunzi waliongeza kiambishi {-*ag*-} kwenye mzizi wa kitenzi (**ilikuwaga*><*ilikuwa,* **balichezaga*><*walicheza*). Kiambishi {-*ag*-} kisichotokea katika Kiswahili sanifu huwa ni cha kawaida katika Kiswahili kitumikacho katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Burundi kikidhihirisha hali ya kuendelea kwa tendo (Nshimirimana, 2019:19). Katika sentensi 21 (a), 21 (b) na 21 (c) wanafunzi wameongeza viambishi, hasa vinavyoonesha uwingi wa nomino (**wa mama*><*mama,* **wa baba*><*baba,**wajamani*><*jamani*). Katika lugha za awali za watoataarifa, hoja kwamba katika Ubantu nomino hulazimika kuwa na kiambishi awali huwa ni ya kawaida. Hivyo, nomino yoyote huambikwa kiambishi awali, aghalabu cha wingi. Kwa hiyo, wanafunzi waliathiriwa na lugha zao za awali walipokuwa wanatumia Kiswahili sanifu.

### 5.7 Matumizi ya Viambishi Mbadala

Katika insha zilizotungwa na wanafunzi kulitokea dosari zinazohusiana na matumizi ya viambishi visivyofaa. Viambishi husika hapa ni pamoja na vipatanishi vya ngeli baina ya nomino na vitenzi au nomino na vivumishi. Pia, viambishi vinavyodhihirisha nyakati vilitumiwa na wanafunzi kwa namna ambavyo walifananisha wakati uliopita na hali timilifu, au wakati uliopita muda kidogo. Hebu tutazame mifano ifuatayo:

22. (a) *Banafunzi benye balifika mapema awakuchelewa.
    → Wanafunzi waliofika mapema hawakuchelewa.
    (b) *Bachache bakashuka bengine bakaingia, bengine bako banaelekea shuleni.
    → Wachache wakashuka, wengine wakaingia ambapo wengine walikuwa wanaelekea shuleni.
23. (a) *Asubuhi ya leo nilitoka nyumbani saa moja na dakika hamsini na tano.
    → Leo asubuhi *nimetoka* nyumbani saa 1:55.
    (b) *Kwa miguu, nilichukuwa dakika tano kufika chuoni.
    → Kwa miguu, *nimechukua (nimetumia) dakika tano kufika chuoni.
    (c) *Siku ya leo tulisoma visuri.
    → Leo *tumesoma* vizuri.
    (d) *Nikimaliza nikaenda kuchunga gari la kunileta mjini.
    → *Nilipomaliza nilienda* kusubiria gari la kunipeleka mjini.

Katika 22 (a) na 22 (b) wanafunzi walitumia kiambishi {*ba-*} badala ya {*wa-*}. Sentensi 22 (a) inadhihirisha kuwa ngeli ya kwanza ambayo huwa ni A-WA katika Kiswahili sanifu huwa ni A-BA katika lugha mbalimbali za awali za watoataarifa. Aidha, katika sentensi 22 (b) matumizi ya kiambishi kipatanishi cha nomino na kivumishi {*ba-*} (*bachache><wachache, *bengine><wengine) yalidhihirisha kuwa viambishi ngeli vya aina hii ni {*m-ba*}. Katika 23 (a), 23 (b), 23 (c), na 23 (d) wanafunzi hawakuweza kuweka tofauti baina ya wakati uliopita na wakati uliopita muda kidogo au hali timilifu. Katika Kiswahili sanifu wakati uliopita hudhihirishwa na kiambishi {-*li*-} ambapo wakati uliopita muda kidogo huoneshwa na mofu {-*me*-}. Kwa upande mwingine, Kiswahili cha Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Burundi (mojawapo ya lugha za awali) hutumia {-*me*-} ama kwa wakati uliopita sana au wakati uliopita muda kidogo au hali timilifu. Pia, aina hiyo ya Kiswahili hutumia {-*ka*-} badala ya {-*li*-}. Hivyo, hali hii inahakikisha kuwa wanafunzi wa vyuo vikuu vya Burundi, baada ya kufundishwa nyakati za Kiswahili sanifu aghalabu wakati uliopita, hushindwa kubainisha tofauti za kimatumizi kati ya {-*li*-}, {-*me*-} na {-*ka*-}. Wanafunzi hao hukosea kwa kutumia {-*me*-} badala ya {-*li*-} au {-*li*-} hutumia {-*me*-}, au {-*ka*-} badala ya {-*li*-}. Sentensi 23 (d) ilidhihirisha matumizi yasiyofaa ya kiambishi cha hali ya masharti ya wakati ujao {-*ki*-} (*Nikimaliza><nilipomaliza). Pia, matumizi ya kiambishi cha hali ya mfuatano wa matendo {-*ka*-} badala ya {-*li*-} kuonesha

wakati uliopita (*_nikaenda><nilienda_) yalidhihirisha kutotambua uamilifu wa viambishi hivyo kwa wanafunzi watumiapo Kiswahili sanifu kutokana na mifumo ya kisarufi iliyojenga uzoefu akilini mwao.

### 5.8 Ugeuzaji wa Viambishi Tegemezi kuwa Maneno

Dosari kuhusiana na ugeuzaji wa viambishi tegemezi kuwa neno zilipatikana katika insha zilizotungwa na wanafunzi. Katika lugha za awali, ipo mifumo inayohusisha maneno halisi pale Kiswahili sanifu kinapotumia viambishi. Kwa upande mwingine, ngeli za mahali {mu-}, {pa-}, na {ku-} zinapotumika zinaweza kuambikwa nomino (Kipacha, 2002). Hivyo, hali hii ilisababisha wanafunzi kukosea watumiapo Kiswahili sanifu kama inavyodhihirika katika sentensi zifuatazo:

24. (a) *Nikabebа watoto _ku masomo_.
    → Nikawapeleka watoto _shuleni_.
    (b) *Gufika hapa _ku chuo_, tena niliwanza masomo yangu ya leo.
    → Nilipofika hapa _chuoni_, nimeanza tena masomo yangu ya leo.
    (c) *Nikarudi (...) _mu kurudi_ nikakutanana najirani yangu.
    → Nikarudi (...) _niliporudi_ (_Katika kurudi_) nikakutana na jirani yangu.
25. (a) *Banafunzi benye balifika mapema awakuchelewa.
    → Wanafunzi _waliofika_ mapema hawakuchelewa.
    (b) *Nikaona na wagonjwa wenye waliombewa.
    → Nikaona wagonjwa _walioombewa_.
26. (a) *Ndo akatusomea alitufundisha vizuri.
    → Ndipo alipotusomea na kutufundisha vizuri.
    (b) *Njo ivo safari yangu imeendeka.
    → Hivyo ndivyo safari yangu ilivyotokea.

Katika 24 (a), 24 (b) na 24 (c) wanafunzi walitumia viambishi ngeli vya mahali _ku-_ na _mu-_ kabla ya nomino za kawaida _masomo_ (shule) na _chuo_, na nomino ya kitenzi jina _kurudi_. Kulingana na mifumo sahihi ya Kiswahili sanifu, wanafunzi walitumia ngeli hizo pamoja na nomino badala ya vielezi vya mahali (*_ku masomo=ku shule_><_shuleni,_ *_ku_ chuo><chuoni). Aidha, wanafunzi walitumia ngeli ya mahali _mu-_ badala ya kirejeshi cha mahali {-_po_-} (_mu kurudi_ ><_niliporudi_) kumaanisha wakati tendo lilipotendeka. Katika 25 (a) na 25 (b), athari nyingine ya lugha za awali ilijitokeza katika tungo za wanafunzi watumiapo Kiswahili sanifu. virejeshi ama viliachwa au kuwakilishwa na kiambishi {-_enye_} kilichoambikwa kiambishi ngeli kutokana na nomino husika (*_benye_ balifika><_waliofika_, *_wenye_ waliombewa>< _walioombewa_). Badala ya kiambishi rejeshi -_o_- wanafunzi walitumia kanuni ya kisarufi ya Kiswahili cha Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Burundi ihusishayo neno -_enye_. Katika 26 (a) na 26 (b), wanafunzi walitumia kanuni ya aina hiyo ya Kiswahili ihusishayo maneno _ndo_ na _njo_ badala ya virejeshi (*_ndo_><_ndipo alipotusomea_, *_Njo_><_Hivyo ndivyo_).

### 5.9 Ukataji na Uunganishaji wa Maneno bila Kuzingatia Utaratibu

Katika kazi za kimaandishi ilibainika kuwa wajifunzaji wanakata maneno mahali pasipofaa au kuunganisha maneno visivyo. Katika maandishi, inambidi mwandishi husika kuzingatia mipaka kati ya neno moja na jingine ili kutowaletea utata wasomaji. Maneno mawili au zaidi yakiunganishwa, hujitokeza kama istilahi mpya lakini isiyo na maana yoyote. Aidha, maneno yasikatwekatwe mahali pasipofaa ili yasipoteze ujumbe unaotarajiwa. Sentensi zifuatazo hudhihirisha dosari za kuunganisha na kukata maneno visivyo:

27. (a) *Mtu mwenye elimu *ana fanya* kazi nzuri sana.
    → *...anafanya...*
    (b) *Elimu *ina saidia* kuondoa ujinga.
    → *...inasaidia...*
    (c) *Mtu *aliye elimishwa* ni mtu muhimu sana.
    →*...aliyeelimishwa...*
    (d) **Juma pili* *nilipo kuwa* kanisani, niliona kiongozi akiwa *ana hubiri*.
    → *Jumapili nilipokuwa...anahubiri*.
28. (a) *Piya inasaidiya mtu namna *yakuishi* na wengine katika jamii yake.
    → *...ya kuishi...*
    (b) *Elimu ni msingi *wamaisha* ama *wakutafuta* maisha.
    → *wa maisha... wa kutafuta...*
    (c) **Katikamaisha* ya kila siku elimu huwa ni muhimu.
    → *Katika maisha ...*
    (e) *Husaidiya watu *kwakujenga* msingi wa maisha.
    → *...kwa kujenga...*

Katika sentensi 27 (a), 27 (b), 27 (c) na 27 (d) maneno sita (6) yalikatwa mahali pasipofaa. Miongoni mwa maneno haya, matano ni vitenzi (**ana fanya*><*anafanya*, **ina saidia*><*inasaidia*, **aliye elimishwa*><*aliyeelimishwa*, **nilipo kuwa*><*nilipokuwa*, **ana hubiri*><*anahubiri*); na neno changamani **Juma pili*><*Jumapili*. Uchunguzi wa data ulidhihirisha kuwa wanafunzi kutoka nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo hukata maneno pasipofaa. Pia, ilionekana kuwa vitenzi hukatwa kwa jinsi ambavyo viambishi tamati na shina la kitenzi hubainika kama mafungu mawili tofauti. Aidha, katika maneno changamani yaundwayo kwa mofu changamano, hutenganishwa kama mafungu mawili tofauti. Katika sentensi 28 (a), 28 (b), 28 (c) na 28 (d), baadhi ya maneno yaliandikwa kwa kuunganishwa (**yakuishi*><*ya kuishi,* **wamaisha*><*wa maisha,* **wakutafuta*><*wa kutafuta,* **Katikamaisha*><*Katika maisha,* **kwakujenga*><*kwa kujenga*). Uchunguzi wa maandishi ya wanafunzi wanaojifunza Kiswahili sanifu ulidhihirisha kuwa maneno yaliyounganishwa huwa ama kiunganishi na neno jingine (*ya kuishi, wa maisha, wa kutafuta*) au kihusishi na neno jingine (*Katika maisha, kwa kujenga*). Hivyo, kwa kuunganisha maneno

visivyo au kukata maneno pasipofaa, maana hupotea kwa sababu viambishi vilivyopatikana havitoi maana yoyote katika lugha ya Kiswahili.

**5.10 Matumizi ya Msamiati Usio Sahihi**

Dosari za msamiati usiosahihi hutokea pale ambapo mwanafunzi hufananisha maneno ambayo si visawe na ambayo hayana uhusiano wowote katika muktadha fulani. Dosari za aina hii zinapotokea, ujumbe unaotarajiwa hupotoshwa kwa sababu maneno yanapobadilishwa, maana za maneno nazo hubadilika. Mifano ifuatayo ilinukuliwa kutoka katika insha za wanafunzi:

29. (a) *Tunapata faida nyingi (...) kama vile *kujishika* (vizuri) maishani.
→ ...*kujitunza* maishani.
(b) *Nikimaliza nikaenda *kuchunga* gari la *kunileta* mjini.
→ ...*kusubiria*...*kunipeleka.*
(c) *Inatubidi *tuwe tunatekeleza* mafundisho ya wazazi na walimu.
→ Inatubidi *kuzingatia/kufikiria*...

Kutokana na sentensi 29 (a) na 29 (b) wanafunzi walitumia msamiati uliopo katika lugha ya Kiswahili na kuupa maana nyingine ambayo ni ya kawaida. Katika 29 (a) kitenzi *kujishika* kilitumiwa pale ambapo Kiswahili sanifu hutumia *kujitunza.* Vilevile, katika 29 (b), kitenzi *kuchunga (gari)* kilitumiwa badala ya *kusubiria gari*. Katika 29 (c), wanafunzi walitumia msamiati *kutekeleza* (kuzama katika mawazo) ambao sasa hujitokeza badala ya kitenzi *kufikiria*. Aidha, katika sentensi hiyohiyo wanafunzi hawakubainisha tofauti kati ya *kupeleka* (kitu mahali fulani) na *kuleta* (kitu kutoka mahali fulani). Mifano iliyojadiliwa hapa ilidhihirisha kuwa msamiati wa lugha za awali uliathiri msamiati wa Kiswahili sanifu.

**6.0 Hitimisho**

Makala hii imechunguza na kuweka bayana aina za dosari zinazofanywa na wanafunzi baada ya kufundishwa kozi mbalimbali zinazohusiana na Kiswahili sanifu katika vyuo vikuu vya Burundi. Uchunguzi ulidhihirisha dosari za aina nne ambazo ni za kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Dosari hizo zilijitokeza katika namna kumi na mbili tofauti. Kutokana na matokeo yaliyowekwa bayana na makala hii, imedhihirika kuwapo kwa hatua ambayo bado haijafikiwa katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika vyuo vikuu vya Burundi, ingawa vyuo vyote vilihimizwa kuleta mchango katika kuendeleza matumizi ya lugha ya Kiswahili nchini. Hivyo, tahadhari haina budi kuchukuliwa kwa wanafunzi na walimu ili kufikia hatua mwafaka ya matumizi sahihi ya Kiswahili sanifu.

**Marejeleo**

Ame, P.M. (2017). Athari za Kiisimu za Lahaja ya Kitumbatu katika Kiswahili Sanifu Kinachotumika katika Shule za Tumbatu Zanzibar. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Aruba, B.K. (2017). Makosa ya Kisemantiki katika Mawasiliano Andishi ya Kiswahili ya Wanafunzi wa Shule za Upili nchini Kenya: Mfano wa Kaunti ya Kakamega. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

Bundalla, R.R. (2017). Athari ya Kimakunduchi katika Kiswahili. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Casco, J.A.S. (2007). "Standard Swahili: Is it Still a Prevailing Category?" *Cuadernos deTrabajo del Centro de Estudios de Asia y África.* Juz. 12: 120-134.

Cioroianu, C.E.B. (2015). "Analysis of Frequent Errors while Learning Romanian as Foreign Language." Katika *Annals of the University of Craiova*. Juz. 1: 33-41.

Corder, S.P. (1973). *Introducing Applied Linguistics*. Middlesex: Penguin.

________(1981). *Error Analysis and Interlanguage*. Oxford: Oxford University Press.

Corder, S.P. na Allen, J.P.B. (1974) *Techniques in Applied Linguistics*. London: Oxford University Press.

Chepkwony, C.L. (2011). Matatizo ya Kisarufi Miongoni mwa Wanafunzi wa Kikipsigis Wanaojifunza Kiswahili Sanifu: Mtazamo wa Lugha Kadirifu. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Fries, C.C. (1945). *Teaching and Learning English as a Foreign Language*. Ann Arbor & Michigan: University of Michigan Press.

Jabeen, A., Kazemian, B. na Shahbaz, M. (2015). "The Role of Error Analysis in Teaching and Learning of Second and Foreign Language". *Education and Linguistics Research.* Juz. 1(2):52-62**.** Inapatikana katika http://dx.doi.org/10.5296/elr.v1i1.8189. Ilisomwa tarehe 21 Novemba 2020.

KAKAMA (2019). *Capacity Assessment of the Development and Use of Kiswahili in the EAC*. Zanzibar: EAKC.

Kipacha, A. (2002). *Lahaja za Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Lado, R. (1957). *Linguistic Across Cultures*. Michigan: The University of Michigan Press.

Lee, E.P. (2001). "Error Analysis on Medical Students' Writing". *ITUA.* Juz. 2: 23-35. Inapatikana katika http://www.stc.arts.chula.ac.th/. Ilisomwa tarehe 21 Oktoba 2020.

Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya Lugha, Isimu na Nadharia. Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publisher (T) Ltd.

Mpangala, G. (2018). Athari ya Lugha ya Kimakonde katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Nshimirimana, E., Misago, M.J. na Tuyubahe, P. (2019). "Le morphème -ag- dans le Kingwana." *ODISSEIA*. 5(1): 1-21. Inapatikana katika http://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0. Ilisomwa tarehe 20 Juni 2020.

Ntawiyanga, S. (2018). Changamoto za Kimofosintaksia Miongoni mwa Wanafunzi wa Kiswahili wa Shule za Upili Wilayani Muhanga, nchini Rwanda. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Nyanda, G. (2015). *Athari za Lugha ya Kinyamwezi katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili.* Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Oduor, C. (2017). "Athari za Uhamishaji wa Sarufi ya Kiluo kwenye Upatanisho wa Sarufi ya Kiswahili." *Kiswahili*. Juz. 76: 100-111.

Richards, J. (1974). *Error Analysis and Second Language Strategies*. London: Longman.

Selinker, L. (1972). *Inter Language*. New York: Rawlence Erlbaum Associates.

Zhang, S. (2007). "Analysis and Classifications of Common Errors in Spoken and Written English Caused by Chinese University Students' Lack of English Grammatical Knowledge." *US-China Foreign Language.* Juz. 5(5):1-5.